

Uzima

Toleo la 12

hello@dignityonline.org.uk

+447340 573 937

Kanisa la Kila Mtu!

Kanisa la Kila Mtu!

Katika kuzuru kijiji kimoja kaskazini mwa Zambia, baadhi yetu walikumbana na nguvu ya ajabu ya Injili inayounganisha. Katika eneo lile makanisa yalikuwa na ubaguzi. Walijitenga kivyao na hawakutaka kutangamana kivyovyote na wale walioitwa “wenye dhambi” katika eneo hilo. Kwa sababu hiyo watu hawakuwahi kusikia ujumbe wa injili. Wale wenzetu walizungumza na watu kuhusu Yesu, wakiwaeleza kuwa Yesu aliwapenda, alikufa kwa ajili yao na kwamba kulikuwa na nafasi yao katika kanisa lake. Mapokezi yalikuwa ya ajabu. Watu ambao kwa kawaida walitengwa, walielekea kwa viongozi wa kanisa na wakadai kuwa walistahihili kuhusika kanisani huku wakisema, “Yesu anatumpenda na anataka tuje kanisani!”

Katika Yohana 1:12 Yohana anaandika, “Bali wote waliompokea, ndio wale waliaminio jina lake, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu.” Yohana anasema Mungu ni wa kila mmoja na kila mmoja ana haki ya kuwa sehemu ya jamii yake. Vitu vyote vinavyotutenganisha, viziwi vyote tunavyoviweka kati yetu haijalishi. Havina nafasi katika kanisa la Mungu. Sote ni wamoja ndani ya Yesu.

Wakati mwingine tunawahukumu watu, tunadhani hawafai kutumiwa na Mungu. Tukifanya hivyo tunakosa kuielewa neema ya Mungu. Tunasahau kwamba pia sisi wakati mmoja tulikuwa watenda dhambi na kuwa kwa hakika sote tunahitaji kwa shauku kuu uzima wa Mungu. Ndio maana kila mtu anafaa kukaribishwa kwenye Vikundi vyetu vya Uzima na makanisani kwetu, hata wale tunaowadhania kuwa “waovu.” Hapana hata mtu mmoja katika dunia ambaye Mungu hawezi kumtumia kwa njia za ajabu na kwa utukufu wake.

Pia tunaweza kuwadharau waumini wengine kwa sababu imani yao inatofautiana na yetu. Wanaweza kwenda kanisa tofauti, kuomba kwa namna tofauti au wanaamini vitu tofauti kiasi na vyetu. Katika Ufunuo 7:9, kuna picha ya watu wa Mungu kama “kusanyiko kuu” kutoka “kila taifa, kabila, watu na lugha.” Kuna utofauti mkubwa kwa watu wa Mungu na hivyo tusitarajie kila muumini kuwa kama sisi. Yesu alituita, kanisa lake, kwa umoja. Tunafaa kuhakikisha kama waumini tunasimama pamoja na kutenga nafasi kwa kila mmoja kwa Kanisa lake.

Zingatia!

Fikiria juu ya eneo unaloishi, ni watu gani ambao wametengwa na kubaguliwa kutoka kanisani? Ni watu gani ambao hawajawahi kusikia kuhusu upendo wa Yesu? Ni watu gani ambao wanahisi hawawezi kukaribishwa kanisani? Andika majina ya baadhi ya watu hawa na muwaombe. Katika wiki ijayo, wakaribishe kwa Kikundi chako cha Maisha. Jitahidi kuwasidia wahisi wamekaribishwa na wanapendwa.

Omba:


- 1) Mungu atajionyesha kwa watu hawa jinsi alivyo.
- 2) Mungu atakupa nafasi kuwaonyesha upendo wake.



“Palikuwa na mtu mmoja, mchawi, na alikuwa amefukuzwa kijijini. Hata washirika wa kanisa walimwogopa. Niliwaza iwapo kuna mtu ambaye tungemtembelea kwanza wakati tukiwa hapa, ni tunayemzungumzia. Nilimwongelesha kuhusu Mungu.

Alianza kulia na kusema, Kitu kimoja ambacho kimenihuzunisha, hapa watu wananiogopa. Kuna watu wazee ambao huja kuhubiri, wazee kukuliko, lakini hamna mtu ambaye ameniongelesha hadi nikalia. Maneno ambayo umeniongelesha yamenigusa. Mtu alimrudia Mungu.”

- Chafwilai, Zambia



Funzo hili limechochewa na Vipindi 1:
Safari Kijijini.

Kwa zaidi:

dignityonline.org.uk/publications